

MUONGOZO WA USAHIHISHAJI

MTIHANI WA PAMOJA

ELIMU YA DINI YA KIISLAM

KIDATO CHA PILI

SEHEMU A Alama 15

1=1@1=10 Alama

i	li	lii	iv	v	vi	vii	viii	ix	x
C	A	B	A	C	C	C	A	A	C

2=1@1=05 Alama

Orodha A	i	li	iii	iv	v
Orodha B	C	F	A	B	D

SEHEMU B Alama 70

3. Njia za kumjua Mwenyezi mungu

i. Nafasi ya Fitrah (maumbile).

ii. Vipaji vya binadam 5@2=10 Alama

iii. Nafsi ya mwanadamu

iv. Mazingira

v. Wahyi (Ufunuo).

4.a) Stara ya vazi la mwanaume ni kustiri kuanzia kitovu hadi chini ya magoti wakati vazi la mwanamke ni kustiri mwili mzima ukiacha macho na viganja vya mikono =04 Alama

b. Sifa ya vazi la kijana

i. Lisitiri mwili au sehemu yote iliyolazimikakisheria

ii. Lisiwe la kubana kiasi chakuonesha maumbile yake ya ndani/ramani ya mwili

iii. Lisiwe na mapambo nje ya kuvutia uzinifu 5@1=05 Alama

iv. Lisiwe jepesi na kuonesha rangi, ukubwa au shepu ya maungo

v. Vazi la mwanamke lisifanane na vazi la kiume na vazi la kiume lisifanane na vazi la kike.

5. Lengo la kila nguzo Tano za Uislamu

i. . Shahada mbili Kuonesha utii Kwa Allah

ii. Kusimamisha Swala kujikinga na maovu na machafu 5@2=10 Alama

iii. Kutoa zaka kuitakasa nafsi na Mali ya mtoaji

iv. Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhan kwa kumcha mungu

v. Kwenda kuhiji Makka kuwa askari wa Mwenyezi mungu au kujitoa muhanga Kwa ajili ya Allah.

6. a) Masharti ya maiti anayeswaliwa

i. Maiti awe muislamu

ii. Maiti iwe imeoshwa na kukafiniwa 3@1=03 Alama

iii. Maiti iwekwe mbele ya wanaoisalia

b). Sunna Tano za Swala ya maiti

i. Kupanga safu Kwa witri 5@1=05 Alama

ii. Mamuma kuinua mikono kwenye kuleta Takbira

iii. Kuwaombea waislam wote Dua.

iv. Imamu kusimama kati kati ya mwili wa maiti ikiwa ni ya kike na usawa wa mabega kama maiti ni ya kiume.

7. Mafunzo matano ya Suratul ya Lahab kwa jamii ya waislam

i). Adhabu ya Allah itakaposhuka mali na watoto havitakuwa msaada

ii). Mwisho wa wapinzani wa uislamu ni pale adhabu ya Allah itakaposhuka

iii). Nasaba si kitu kitakachopelekea mtu kuokoka na adhabu ya Allah 5@2=10 Alama

iv). Chokochoko za maadui wa uislamu hazitasaidia kuangamiza dini ya Allah

v). Wakubwa wa mji katika eneo lolote ndio wa mwanzo katika kupinga harakati za uislamu

8. a). Maana ya Fiqh.- Ni fani ya elimu ya Kiislamu inayohusiana na ufahamu juu ya kanuni na sheria (hukumu) mbali mbali za ibada na =04 Alama

b. Fiqh ya Ibadat inajushughlisha na mambo ya ibada kama Swala, Zaka, Swaum, Hijja, Ndoa, Talaka, Mirath, wakati Fiqh ya Muamalat – inahusiana na kanuni na sheria kuhusu mambo ya kibinafsi na kijamii; siasa, uchumi, utamaduni.=04 Alama

c.). Misingi ya Fiqh (Vyanzo vya Sheria ya Kiislamu).

1. Qur'an- Ndio chem. chem. kuu ya sheria za Kiislamu. =03marks

ii. Sunnah (Hadith)- Ni msingi wa pili unaotokana na mwenendo wa Mtume (s.a.w) katika kutekeleza maamrishi ya Mwenyezi Mungu (s.w). =03 Alama

iii). Ijtihad (Qiyaas na Ijmaa). Ni hali ya kufanya jitihada katika kufafanua sheria na hukumu mbali mbali za Kiislamu zilizomo katika Qur'an na (Sunnah) Hadithi za Mtume (s.a.w) =03 Alama

9 a). Sifa za muumini wa kweli.

i. Ni yule ambaye imani yake inathibitishwa katika matendo ya kila kipengele cha maisha yake ya kila siku.=01Alama

ii. Ni yule anayejipamba na sifa za waumini zilizoainishwa katika Qur'an na Sunnah katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kila siku.=01Alama

iii. Ni yule anayeendea kila kipengele cha maisha yake kwa mujibu wa vipengele vyote vya nguzo za imani ya Kiislamu. =01 Alama

9 b. Nguzo za matamshi (visomo) katika swala

i.Takbiira ya kuhirimia swala

ii.Kusoma Suratul-Fatihah

iii.Kusoma Tahiyatu

iv.Kumswalia Mtume (s.a.w) 5@1=05 Alama

v.Kutoa Saalam

SEHEMU C ( Alama 15)

Funga –Ni kujizuia katika jambo lolote ambalo mtu amezoea kulifanya AU Ni ibada ambayo inahususha kujizuia,kula,kunywa,kuingiza kitu katika tundu za mwili na kujizuia na maasi yeyote tangu alfajiri ya kweli hadi kuingia magharibu. 1.5 Alama

Umuhimu Wa Funga 5@2.5=12.5 Alama

- Funga ya mwezi wa Ramadhan ni nguzo ya Nne katika Uislamu
- Kufunga mwezi wa Ramadhan ni utambulisho Wa Uislamu

- Kufunga mwezi wa Ramadhan ni amri ya Mwenyezi Mungu (S.W)
- Kufunga mwezi wa Ramadhan ni utambulisho Wa Ucha Mungu wa Mtu
- -Kutofunga mwezi wa Ramadhan makusudi hupelekea kukosa msamaha

Hitimisho 01Alama